**ALIYEUPENDEZA MOYO WA MUNGU**

Alipopata mwaliko, Mtume Paulo aliwahutubia viongozi wa sinagogi katika Matendo 13. Katika hotuba hii, alitoa muhtasari kwa ufupi wa historia ya Israeli tangu kutoka Misri hadi siku za Daudi. Katika mstari wa 22, alimzungumzia Daudi kama mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu. Maneno haya hayazungumzii maisha yote ya Daudi, kwa kuwa yalikuwapo mambo mengine katika maisha yake ambayo hayakuupendeza moyo wa Mungu (1Wafalme 15:5). Na wala haya maneno hayakuwa yanazungumzia tabia ya Daudi. Zaidi ya yote, Daudi hakuwa muasi au kaidi kwa Mungu. Daudi alijionyesha kwamba ni mtu anayeupendeza moyo wa Mungu kwa namna nyingi nyakati za utawala wake. Kwa kuzingatia kwa makini katika namna ya kuyachukua mazuri katika tabia za Daudi, nasi vilevile twaweza kuwa watu wanaoupendeza moyo wa Mungu. Hebu tuangalie katika makala hii ili kuona lililomfanya Daudi awe mtu wa jinsi hii.

**ALILIPENDA NENO MUNGU-ZABURI 119:97**– Kutokana na jinsi alivyolipenda Neno, Daudi alilitafakari muda wote. Mtu anapokipenda kitu fulani, ni vigumu kukiachia. Hivi ndivyo Daudi alivyojisikia juu ya Neno la Mungu, muda wote lilikuwa mbele yake. Kwa kuzingatia hili, leo tunakabiliwa na swali kwamba tunaweka kitu/jambo gani kabla ya Neno la Mungu? Kwa wengi inaonekana kwamba mambo mengine ndiyo yana umuhimu**.** Tuna muda wa kutazama luninga, kufanya kazi za shule, burudani, kazi, na kdha wa kadha, lakini tunakuwa na muda kiduchu au wakati fulani hatuna muda kabisa wa kusoma Neno la Mungu. Wengi wanaoitwa Wakristo wanaweza kunukuu zaidi mambo yatokayo katika elimu dunia kulikoni yatokayo katika Biblia. Mara nyingi wengi wanayatanguliza mbele mambo yasiyo ya kiroho. Wanafahamu mambo ya kihistoria, takwimu za kimichezo, orodha ndefu ya “mambo yasiyofaa”, lakini wana fahamu kiduchu kabisa Neno la Mungu. Watu wanaosema hawawezi kudondoa Biblia huwa nawasikia wakiimba karibia kila neno la kila wimbo maarufu. Hivi wanadhani wanamdhihaki Mungu wanaposema mambo kama haya?

**DAUDI ALILIFICHA NENO LA MUNGU MOYONI MWAKE-ZABURI 119:11–** Akili iko kama kompyuta na ina uwezo wa kuhifadhi kiasi kikubwa cha taarifa. Kwa hivyo, nami nashauri “tuhifadhi” yafuatayo;

Waebrania 10:25….tukijaribiwa kuacha kukusanyika, tutakumbuka panavyosema.
Wakolosai 4:6 ….tukijaribiwa kusema majungu, kutumia lugha chafu tutakumbuka panavyosema .
1 Yohana 3:9...na hatutatenda dhambi.

Tukiweka wigo baina ya ng’ombe na shamba la mahindi, ng’ombe hawezi kula mahindi. Toa wigo na mahindi yataliwa. Ndivyo ilivyo kuhusu dhambi. Endapo tunaweka kitu fulani (Neno la Mungu) baina yetu na dhambi hatutatenda dhambi.

**DAUDI ALIUNGAMA DHAMBI ZAKE– ZABURI 51:3**– Daudi hakuongelea dhambi za wengine au kujaribu kurusha lawama Nathani alipomwendea (2 Samuel 11:2-15, hasa mst.13) Tunatakiwa kuziungama dhambi zetu kama vile Daudi (Yakobo 5:16; 1 Yohana 1:9). Tunatakiwa kutambua kuwa tunawajibika kwa ajili ya makosa yetu tu (Warumi 14:12; 2 Wakorintho 5:10). Kwa kufanya hivi, tutaona haja ya kuyaungama makosa yetu

kwa Mungu ili tuweze kusamehewa.

**DAUDI ALIPENDA KUMTUKUZA MUNGU– ZABURI 139:14**-Daudi alimtukuza Mungu kwa vyombo vya muziki (Zaburi 150) wengi wanadai tuna haki ya kufanya hivyo. Daudi alitoa matoleo ya wanyama na alifukiza uvumba, walakini ni wachache watakaodai kwamba leo tunatakiwa kufanya hivyo hivyo. Ni lazima tupate uhalali kutoka katika Agano Jipya kwa ajili ya matendo yetu (Wakolosai 3:17). Kama hatuwezi kupata uhalali wa Agano Jopya, basi hatuna uhalali wa kufanya mambo kama hayo chini ya Agano Jipya. Daudi alimtukuza Mungu kwa sababu alimjua anayemtukuza. Leo tunatakiwa kumjua Mungu tunayemtumikia ili tumtukukuze vilivyo.

**DAUDI ALIUCHUNGA ULIMI WAKE– ZABURI 39:1**– Ni rahisi kushindwa kuuchunga ulimi. Tunapoenda kumwona daktari anasema "toa ulimi." Ulimi husaidia kugundua maradhi mengi. Hebu fikiria kama Yesu angesema "toa ulimi" angeona nini? Matusi? Majungu? Usingiziaji? Mizaha? Au sifa za kumtukuza? (Yakobo 3:2, 8, 13).

**DAUDI ALIZICHUKIA NJIA ZOTE ZA UONGO– ZABURI 119:104**– Tuonapo neno "ndiyo maana" tunaenda nyuma ili kuona dhamira ya kuwapo kwake mahali hapo. Zingatia kilichosemwa kabla "Kwa mausia yako najipatia ufahamu, ndiyo maana ……" Kama Wakristo tunatakiwa kukichukia anachokichukia Mungu (Mithali 6:16-19; Ufunuo 2:6).

**DAUDI ALUPENDA UMOJA– ZABURI 133:1**– Angalia Daudi anavyosema juu ya umoja. Anasema ni vema na inapendeza. Baadhi ya vitu kama dawa fulani, ni njema lakini hazipendezi. Vitu vingine vyaweza kupendeza lakin si vyema (Waebrania 11:24-26). Kama vile Daudi alivyoupenda umoja, nasi tunatakiwa kufanya vivyo hivyo na kwa kuwa hili ndilo jambo ambalo Yesu aliliombea katika Yohana 17:21-23. Twaweza kutembea pamoja kama itupasavyo kwa kujitahidi tu kuwa katika umoja (Amosi 3:3). Kujitahidi kuwa na umoja ni dalili ya kupendana na kumpenda Mungu. Kufanya vinginenvyo ni dalili ya jambo lingine.

Tunayo fursa ya kwamba tuwe watu ambao "tunaupedeza moyo wa Mungu" kwa njia ya utiifu na uthabiti katika kumtumikia. Hata hivyo, hilo sio swali. Swali ni kwamba tutafanya ambalo litapelekea Mungu atuone kama mtu aupendezaye moyo wake?